**HOTUBA YA MHE. CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA KUHUSU UTEKELEZAJI WA HOJA ZA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 18 JUNI, 2024.**

- **Katibu Tawala wa Mkoa,**
- **Mstahiki Meya wa Manispaa,**
- **Ndg. Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya,**
- **Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,**
- **Waheshimiwa Madiwani,**
- **Mkaguzi Mkuu wa Nje wa Mkoa kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,**
- **Wataalam kutoka Sekretarieti ya Mkoa,**
- **Katibu Tawala wa Wilaya ya Sumbawanga,**
- **Mkurugenzi Mtendaji na Wataalamu wa Halmashauri ya Manispaa,**
- **Wageni Waalikwa,**
- **Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…………. Kazi Iendelee.**

***Mstahiki Meya na Mwenyekiti wa kikao,*** Awali ya yote napenda nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sisi sote kuwa na afya njema. Kwa namna ya pekee nimshukuru na kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa namna anavyoiongoza nchi yetu kwa weledi mkubwa na kuitangaza nchi yetu Kimataifa. Namshukuru **Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassa**n kwa kuendelea kutuletea fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ya Wananchi kwenye Sekta za Afya, Elimu, Miundombinu ya Barabara na Uwanja wa ndege, na Maji.

***Mstahiki Meya,*** Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 imepata Hati Safi (Inayoridhisha). Nichukue nafasi hii kukupongeza wewe Mstahiki Meya, Mkurugenzi pamoja na Wataalam wote wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa kazi nzuri na ushirikiano uliowawezesha kupata Hati Safi. Ni matumaini yangu kuwa mtaendeleza ushirikiano huo huo katika kutekeleza majukumu yenu.

***Mstahiki Meya,*** Naomba sasa nizungumzie masuala yaliyoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwenye taarifa yake kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023.

***Mstahiki Meya,*** Katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2022/2023 iliyotolewa Aprili, 2024 ilionyesha kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ilikuwa na Hoja za miaka ya nyuma ambazo hazijafungwa **28** na Hoja za Mwaka huu wa Ukaguzi (2022/2023) **25** hivyo kufanya Jumla ya Hoja **53** na Maagizo 6 ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) hayajatekelezwa mpaka sasa. Natambua Katibu Tawala Mkoa amekuwa akitoa maelekezo mbalimbali juu ya kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ambayo kwa sehemu kubwa yakifuatwa maelekezo hayo yanazisaidia Halmashauri kupunguza au kuondoa kabisa hoja za ukaguzi. Kupitia Kikao hiki nikuagize Mkurugenzi na Wataalam wako kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Nje kufanya uhakiki ili Hoja hizi ziweze kufungwa na kutekeleza

maelekezo yote yanayotolewa na Katibu Tawala Mkoa kuhusiana na usimamizi wa fedha na masuala ya kiutendaji katika Halmashauri. Pamoja na Hoja hizi yapo masuala ambayo ningependa kuyatolea maelekezo **mahususi baada ya kupitia taarifa yenu ya ukaguzi;**

1. Madeni ya Halmashauri, kwenye taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebainisha madeni ambayo Halmashauri inadaiwa ikiwemo Mishahara ya Watumishi **shilingi 39,513,500.00**, Makato ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSF) **shilingi 81,040,243**, Makato ya Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) **shilingi 1,433,970.00** na Madeni mbalimbali ya Wazabuni na Watoa Huduma yalioneshwa kwenye taarifa ya fedha. Madeni haya yanaleta malalamiko na kuchafua taswira ya Halmashauri na Mkoa kwa ujumla. Nikuagize Mkurgenzi kuhakikisha unaweka mikakati na mipango ya kulipa madeni hayo.
2. Kuhusu Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani, Mkaguzi amebainisha maeneo ambayo Halmashauri haifanyi vizuri katika Ukusanyaji wa mapato ikiwemo kutokusanya mapato kutoka kwenye ushuru wa taka na jitihada ndogo za halmashauri katika kukusanya mapato kwenye vyanzo mbalimbali, nikutake Mkurugenzi kuweka mikakati ya kuhakikisha Halmashauri inakusanya mapato kikamilifu lakini pia kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa zinawasilishwa Benki kwa wakati kama Sheria za Fedha zinavyoagiza. Natambua Katibu Tawala (M) amekwishatoa maelekezo ya marufuku ya kutumia fedha mbichi kupitia barua yake ya **tarehe 02 Mei, 2024**, nami **nasisitiza ni marufuku kutumia fedha mbichi na wote waliohusika wachukuliwe hatua stahiki za kinidhamu na kisheria. Aidha Halmashauri iandae Mkakati wa kuongeza Makusanyo na kuuwasilisha kwa Katibu Tawala Mkoa.**
3. Kwa upande wa Usimamizi wa Miradi, Mkaguzi pia amebainisha mapungufu katika Usimamizi na Ukamilishaji wa Miradi mbalimbali ya maendeleo, nikuagize Mkurugenzi pamoja na timu yako ya Wataalam

kuhakikisha miradi inayotekelezwa inakamilika kama ilivyokusudiwa ili kutimiza azma ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma Stahiki kwa wakati.

4. Serikali imeendelea kufanya maboresho ya Mifumo mbalimbali ikiwemo mfumo wa kukusanyia mapato (TAUSI), Mfumo wa kusimamia mali za Serikali (GAMIS) pamoja na mifumo mingine ya fedha na utawala, Mkaguzi amebainisha mapungufu mbalimbali katika matumizi ya mifumo hiyo. Nikuagize Mkurugenzi kwa kushirikiana na Wataalam kuhakikisha kasoro au dosari zote zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinarekebishwa na kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inatumika kikamilifu.
5. Kwenye Eneo la Manunuzi pamoja na kupungua kwa Hoja kwenye eneo la Manunuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 ukilinganisha na Miaka ya Nyuma, bado kuna mapungufu ambayo Mkaguzi ameyabainisha. Kwa sasa Serikali imeanzisha Mfumo wa Manunuzi wa Kielektroniki (NeST) ni matumaini yangu kuwa Halmashauri inautumia Mfumo huu kikamilifu ambao utaondoa dosari nyingi ambazo Mkaguzi amezibainisha kwenye eneo la manunuzi. Nikutake Mkurugenzi kuhakikisha kuwa mfumo huo unatumika kikamilifu.
6. Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Utengaji wa Fedha kwa ajili ya miradi ya Maendeleo Mkaguzi amebainisha mapungufu katika utekelezaji wa bajeti ikiwemo Halmashauri kutenga fedha pungufu za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo kinyume na miongozo ya Bajeti, vilevile Halmashauri kutumia fedha za ununuzi wa gari la Mstahiki Meya kiasi cha **Shilingi 184,693,826** kwa matumizi mengine ambayo hayakukusudiwa. Nikuagize Mkurugenzi kuhakikisha kuwa Matumizi yote yanayofanyika yanazingatia sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015 na miongozo ya bajeti iliyowekwa na siyo vinginevyo.

***Mstahiki Meya,***Pamoja na maelekezo haya niliyoyatoa kutokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali naomba nitoe maelekezo ya jumla kwa Halmashauri yako ili kupunguza na kuepuka Hoja za Ukaguzi kama ifuatavyo: -

i. Kutoa ushirikiano kwa Wakaguzi wa Nje pindi wanapofanya Ukaguzi badala ya kusubiri Hoja za Ukaguzi na Wakuu wa Idara na Vitengo husika wakatoe maelezo au ufafanuzi kwa wakaguzi badala ya kuwatumia Wasaidizi. Hii itasaidia baadhi ya Hoja kuisha wakati wa Ukaguzi unapoendelea.
ii. Halmashauri ihakikishe inaongeza wigo wa makisio ya mapato ya ndani kwa kuwa wabunifu wa kutafuta vyanzo vipya badala ya kutegemea vyanzo vile vile ambavyo haviongezi tija na kuhakikisha kuwa inatumia mifumo mbalimbali ya Kieletroniki katika kudhibiti utoroshaji wa mapato, Vilevile watumishi wasio waadilifu katika eneo la ukusanyaji wa mapato wachukuliwe hatua stahiki kwa wakati bila kuchelewa;
iii. Halmashauri iimarishe usimamizi wa Miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa kupitia fedha za mapato ya ndani na zile za Serikali Kuu ili ikamilike na kutoa huduma zilizokusudiwa na Serikali.
iv. Utekelezaji wa maelekezo haya pamoja na kuwasilisha mpango wa utekelezaji wa Hoja uwasilishwe Ofisi ya Katibu Tawala (M) kabla ya tarehe 26 Juni 2024 ili taarifa hizi ziunganishwe na kutumwa TAMISEMI kabla tarehe 30 Juni 2024.

***Mstahiki Meya,*** Mwisho, Napenda kukushukuru tena wewe pamoja na Waheshimiwa Madiwani na timu ya Menejimenti ya Halmashauri kwa kunialika kuhudhuria kwenye kikao hiki muhimu. Aidha zoezi la uandikishaji wa wapiga kura kwaajili ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 Waheshimiwa Madiwani hamasisheni Wananchi kujitokeza kwa wingi ili mwakani watumie haki yao ya Kidemokrasia. Aidha mwaka huu 2024 kutakuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Nawaomba tuwahamasishe wananchi kujitokeza kuchagua viongozi wao muda utakapo fika.

Mungu Ibariki Tanzania,

Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,

Mungu Bariki Manispaa ya Sumbawanga.

Asanteni sana kwa Kunisikiliza.

Mhe. Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA RUKWA**